JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

# Muundo na Majukumu ya Serikali za Mitaa

# Yaliyomo UK


| | |
|---|---|
| Utangulizi | 1. |
| Maana ya Serikali za Mitaa na Dhana ya kupeleka Madaraka kwa Wananchi | 2 |
| Mfumo na Muundo wa Serikali za Mitaa | 3 |
| Mamlaka za Wilaya | 3 |
| Mamlaka za Miji | 5 |
| Muundo wa Serikali za Mitaa mbalimbali | 6 |
| Kitongoji | 6 |
| Mtaa | 6 |
| Kijiji | 7 |
| Kamati ya Maendeleo ya Kata | 7 |
| Mamlaka ya Mji Mdogo | 8 |
| Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Jiji (kama vile Mwanza) | 8 |
| Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam | 9 |
| Majukumu ya Serikali za Mitaa | 10 |
| Majukumu ya Wananchi | 10 |
| Majukumu ya Mkutano Mkuu wa Kitongoji | 11 |
| Wajibu na Majukumu ya Mkutano Mkuu wa Mtaa | 11 |
| Wajibu na Majukumu ya Mkutano Mkuu wa Kijiji | 12 |
| Majukumu ya Kamati ya Maendeleo ya Kata | 12 |
| Majukumu ya Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Jiji | 13 |
| Hitimisho | 14 |

# Utangulizi

Lengo kuu la kijitabu hiki ni kuongeza ufahamu kwa wananchi juu ya mfumo wa Serikali za Mitaa wa Tanzania na majukumu yake kwa mujibu wa Sheria. Ufahamu huu utaboresha kwa kiasi kikubwa ushiriki na michango ya wananchi na wadau mbalimbali katika maendeleo, na hasa katika ngazi za msingi.

Kijitabu hiki kinaainisha kwa lugha ya kawaida maana ya Serikali za Mitaa kwa mfumo wa Tanzania na kuorodhesha majukumu ya ngazi mbalimabli zinazounda mfumo huo, kama ilivyoainishwa katika Sheria na nyaraka mbalimbali za Serikali. Kwa kupitia kijitabu hiki mwananchi anaweza kuelewa muundo, majukumu na wajibu wa Halmashauri zake na hivyo kuweza kuitumia kikamilifu zaidi fursa inayotolewa na mfumo huu. Izingatiwe kuwa kijitabu hiki si tafsiri halisi ya sera na Sheria husika bali ni tafsiri rahisi inayolenga kuongeza ufahamu wa mfumo wenyewe. Hivyo basi kwa ufahamu wa undani zaidi ni vizuri msomaji akawasiliana na Halmashauri yake ili apate nyaraka husika kama vile Katiba ya Tanzania, Sheria ya Serikali za Mitaa, nakadhalika.

# Maana ya Serikali za Mitaa na Dhana ya kupeleka Madaraka kwa Wananchi

Yafuatayo ni maelezo mafupi kuhusu maana ya Serikali za Mitaa kwa kuzingatia dhana ya kupeleka madaraka kwa wananchi.

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inafafanua kuwa Serikali za Mitaa ni vyombo vya wananchi vilivyopo katika ngazi ya msingi ya Serikali. Serikali za Mitaa huundwa , huendeshwa, husimamiwa na kuwajibika kwa wananch wenyewe. Hivyo basi Serikali za Mitaa zimeundwa kwa mantiki ya kuwawezesha wananchi, wanaume kwa wanawake, kushiriki katika masuala ya siasa, uchumi, upatikanaji wa huduma na utawala katika maeneo yao na katika nchi yao. Kwa ujumla ni muundo ambao unawawezesha wananchi kuwa na udhibiti wa maamuzi ya wawakilishi waliowachagua. Kwa mtazamo huu wa kikatiba, Serikali za Mitaa ni fursa kubwa kwa wanajamii kukuza demokrasia na ushiriki wao katika maendeleo ya maeneo yao. Ni vyema ieleweke kuwa Serikali za Mitaa si wakala wa Serikali Kuu bali ni serikali kamili zenye mamlaka chini ya Sheria. Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wananchi ndio msingi wa mamlaka yote na Serikali inapata madaraka na mamlaka yake yote kutoka kwa wananchi. Hii ndiyo maana hasa ya kupeleka madaraka kwa wananchi.

# Mfumo na Muundo wa Serikali za Mitaa


Sheria Namba 7, 8 na 9 kama zilivyopitishwa na Bunge mwaka 1982 na kurejewa tena mwaka 1999 na 2000, zinatoa maagizo juu ya uundaji, uendeshaji na usimamizi wa Serikali za Mitaa. Kuna mifumo miwili ya Serikali za Mitaa katika Tanzania. Kuna mfumo wa Mamlaka za Wilaya na ule wa Mamlaka za Miji. Yafuatayo ni maelezo mafupi juu ya mifumo hiyo miwili, tukiazja na ule wa mamlaka za wilaya.

## Mamlaka za Wilaya

Mamlaka za wilaya ni pamoja na Halmashauri za Wilaya, Mamlaka za Miji Midogo, Kamati za Maendeleo za Kata (WDC), Serikali za Vijiji na Vitongoji. Halmashauri za Wilaya, Mamlaka za Miji Midogo na Serikali za Vijiji ni vyombo vyenye madaraka ya kiutawala ya juu kabisa katika maeneo yake. Maeneo yaliyo chini ya Halmashauri za Wilaya yamegawanywa katika Kata ambazo ndiyo majimbo ya uchaguzi wa Madiwani. Kamati za Maendeleo za Kata na Vitongoji zina kazi ya kuratibu shughuli za maendeleo na za ulinzi katika maeneo husika.

Kuundwa kwa vitongoji ni mojawapo ya marekebisho yaliyofanywa siku za karibuni ili kuboresha muundo wa Serikali za Mitaa. Lengo la kuanzisha vitongoji ni pamoja na kuimarisha demokrasia kwa wananchi, na kuziba pengo lililoachwa baada ya kuondolewa wajumbe wa nyumba kumikumi waliokuwa chini ya mfumo wa chama kimoja cha kisiasa. Kuwepo kwa vitongoji kunatoa fursa kwa wananchi kushiriki moja kwa moja katika siasa ya vyama vyingi kwa ngazi ya msingi kabisa. Ni jambo la kawaida kukuta kuwa wenye -viti wa vitongoji mbalimbali katika kijiji kimoja wanatoka kwenye vyama tofauti vya siasa.


Kielelezo Namba 1: Mfumo wa Serikali za Mitaa chini ya Mamlaka za Wilaya



## Mamlaka za Miji

Mamlaka za Miji ni pamoja na Halmashauri za Jiji, Halmashauri za Manispaa, Halmashauri za Miji, Kamati za Maendeleo za Kata, Serikali za Vijiji, Mitaa na Vitongoji. Maeneo yaliyo chini ya Halmashauri za Miji yamegawanywa katika kata ambayo ndiyo majimbo ya uchaguzi wa Madiwani. Kamati za Maendeleo za Kata na Mitaa na Vitongoji hazina madaraka kamili ya kisiasa na kiutawala kama halmashuri za miji bali zina majukumu ya kuratibu shughuli za maendeleo. Kama ilivyo katika mfumo wa Mamlaka za Wilaya, lengo la kuundwa kwa Mitaa na Vitongoji ni pamoja na kuimarisha demokrasia kwa wananchi .

Kielelezo Namba 2: Mfumo  wa Serikali za Mitaa chini ya Mamlaka za Miji



# Muundo wa Serikali za Mitaa mbalimbali

Baada ya kuufahamu mfumo ni vizuri sasa tukaangala muundo wa Serikali za Mitaa tukiwa na maana ya ni akina nani wanaunda Serikali hizo, namna amawanavyochaguliwa, kuteuliwa au kuajiriwa. Tunaanza na wale wajumbe wa ngazi ya msingi kabisa, yaani Kitongoji.

## Kitongoji

Kitongoji ni sehemu ya kijiji au mji mdogo, kama inavyoamriwa na Halmashauri husika. Hakuna idadi maalumu ya kaya katika kuunda kitongoji, bali inategemea mapendekezo ya Serikali ya Kijiji husika na kuidhinishwa na Halmashauri ya Wilaya husika. Muundo wa utawala katika ngazi ya Kitongoji unajumuisha :

- Mkutano Mkuu wa Kitongoji unaojumuisha wakazi wote wenye umri usiopungua miaka 18 na wenye akili timamu.
- Mwenyekiti wa Kitongoji ambaye anachaguliwa na Mkutano Mkuu wa Kitongoji.
- Kamati ya Kitongoji inayojumuisha wajumbe wasiopungua wawili na Katibu. Wote huteuliwa na Mwenyekiti

Kama tunavyofahamu, shughuli nyingi za utekelezaji zinafanyika katika ngazi ya Kitongoji, na hivyo basi ni muhimu wajumbe wa Kamati ya Kitongoji wakawa na uwezo wa kuhamasisha wananchi.

## Mtaa

Kama inavyosomeka hapo juu, Mtaa ni sehemu ya Kata na ni ngazi ya Serikali za Mitaa katika Mamlaka za Miji. Hakuna ngazi nyingine chini ya Mtaa.  KiSheria kila Mtaa unapaswa uwe na kaya zisizopungua 50.

Muundo wa kamati ya Mtaa ni kama ifuatavyo:

- Mkutano Mkuu wa Mtaa.
- Mwenyekiti wa Mtaa ambaye anachaguliwa na Mkutano Mkuu wa Mtaa.
- Kamati ya Mtaa yenye wajumbe wasiozidi sita watakaochaguliwa na Mkutano Mkuu. Kati ya hao wajumbe wawili wawe wanawake. Katibu huchaguliwa na Mwenyekiti.

- Kuna baadhi ya Kata za Halmashauri ambazo zimeajiri maafisa watendaji wa Mitaa ambao wanamsaidia Mwenyekiti.

## Kijiji

Serikali ya Kijiji huundwa katika kijiji kilichoandikishwa kisheria. Kiwango cha chini cha kaya katika kijiji isipungue 250, na wala wakazi wake hawapungui 1250. Idadi hii ni muhimu ikazingatiwa kama kiwango cha chini ili kuhakikisha kuwa idadi ya watu katika kijiji inaweza kutosheleza huduma zinazotolewa katika ngazi hiyo.

Muundo wa kamati ya Kijiji ni kama ifuatavyo:

- Mkutano Mkuu wa Kijiji ukijumuisha wakazi wote wasiopungua umri wa miaka 18 na wenye akili timamu.
- Mwenyekiti wa Kijiji ambaye anachaguliwa na Mkutano Mkuu wa Kijiji
- Wenyeviti wa Vitongoji.
- Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji ambao ni kati ya 15 na 25 na wataunda kamati mbalimbali kuzingatia mahitaji na vipaumbekle vya Kijiji.
- Afisa Mtendaji wa Kijiji.

Tunasisitiza kwamba kiSheria Mkutano Mkuu wa Kijiji ndiyo mamlaka yenye madaraka ya juu kabisa kijijini na ndiyo yenye wajibu wa kuwachagua na kuwaondoa madarakani wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji.

## Kamati ya Maendeleo ya Kata

Kata ni sehemu ya Halmashauri na huundwa na Halmashauri husika kwa kupitia kwa Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa.

Kwa mujibu wa Sheria kila Kata itakuwa na Kamati ya Maendeleo ya Kata ambayo itakuwa na Wajumbe wafuatao:

- Diwani ambaye ni mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Kata.
- Wenyeviti wa vijiji vyote katika kata hiyo.
- Diwani wa viti maaulumu mkazi wa Kata husika.
- Watu walioteuliwa na Kamati ya Maendeleo ya Kata kutoka mashirika yasiyo ya Kisenkali (NGOs) au vikundi vya kiraia, kama

vile wanawake, vijana, walemavu, nk. lakini hawaruhusiwi kupiga kura.

- Afisa Mtendaji wa Kata kama Katibu.

## Mamlaka ya Mji Mdogo

Sheria Namba 6 ya mwaka 1999 inabainisha muundo wa Mamlaka ya Mji Mdogo kama ifuatavyo:

- Mwenyekiti ambaye atachaguliwa miongoni mwa wenyeviti wa vitongoji vilivyo katika eneo la Mji Mdogo husika.
- Wenyeviti wa vitongoji vilivyo katika eneo la Mji Mdogo husika.
- Wajumbe wasiozidi watatu walioteuliwa na Halmashauri ya Wilaya ambayo huo Mji Mdogo upo chini yake.
- Mbunge anayewakilisha jimbo ambamo mamlaka hiyo imo.
- Wajumbe viti maalumu ambao hawatapungua robo ya wajumbe waliotajwa hapo juu.

## Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Jiji (kama vile Mwanza)

Halmashauri za Miji, Manispaa au Jiji zinaundwa na wajumbe wafuatao:

- Madiwani wa kuchaguliwa kutoka kata zilizomo kwenye mji, manispaa au jiji husika.
- Wabunge wanaowakilisha majimbo ya uchaguzi yaliyomo ndani ya mji, manispaa au jiji husika.
- Wabunge wa kuteuliwa.
- Madiwani viti maalumu wasiopungua theluthi ya wajumbe wote.
- Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji, Manispaa au Jiji kama Katibu.

## Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam

Sheria Namba 8 ya 1982, kama ilivyorekebishwa na Sheria Namba 6 ya mwaka 1999, inafafanua muundo wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kama ifuatavyo:

- Meya aliyechaguliwa na Madiwani wa mamlaka za miji zilizo ndani ya eneo la Halmashauri ya jiji hilo.
- Naibu Meya wa kuchaguliwa kama ilivyoelezwa hapo juu, lakini asiwe anatoka katika Halmashauri ile anayotoka Meya.
- Wabunge wote wa kuchaguliwa, na angalau wabunge wawili wanawake walioteuliwa kutoka wabunge wanawake wanaoishi ndani ya jiji husika.
- Madiwani watatu kutoka kila Halmashauri na mmoja lazima awe mwanamke.
- Meya wa kila Halmashauri katika jiji hilo.
- Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji kama Katibu.

# Majukumu ya Serikali za Mitaa

Majukumu ya Serikali za Mitaa yanaangukia sehemu kuu nne, nazo ni:

(a) Kuwezesha na kudumisha utulivu, amani na utawala bora.
(b) Kudumisha upatikanaji wa huduma mbalimbali za kijamii na miundo mbinu.
(c) Kuchochea maendeleo ya kiuchumi na kijamii.
(d) Kulinda mazingira kwa lengo la kuchangia katika maendeleo endelevu.

Utekelezaji wa majukumu haya unategemea jinsi ambavyo ngazi mbalimbali katika Serikali za Mitaa zinavyotekeleza wajibu na majukumu katika mfumo wote wa Serikali za Mitaa ili kuongeza uelewa wa majukumu hayo hasa kwa wananchi. Ufuatao ni muhtasari wa majukumu ya ngazi mbalimbali za Serikali za Mitaa.

Kwa kuwa lengo kuu la muhtasari huu ni kuongeza ufahamu miongoni mwa wananchi, basi tunazingatia majukumu yale ya mikutano mikuu ya Kitongoji, Mtaa, Kijiji, Kata na Halmashauri kwa vile mwananchi anaweza kushiriki moja kwa moja katika mikutano hiyo. Ni vyema basi akajua majukumu na uwezo wa vikao hivyo. Kabla ya kuelezea majukumu katika ngazi ya Kitongoji, tunagusia kwa ufupi tu majukumu ya wananchi katika mfumo mzima wa Serikali za Mitaa.

## Majukumu ya Wananchi

Kisheria na kiutawala wananchi wanatarajiwa kutekeleza majukumu yafuatayo:

- Kuelewa Sheria zote zinazohusu Serikali za Mitaa na kuishi kufuatana na Sheria hizo.
- Kutambua nafasi yake katika jamii na kushiriki katika shughuli mbalimbali za maendeleo.
- Kudai haki zake za msingi kutoka kwa viongozi wake.
- Kuhakikisha kuwa viongozi wanatimiza wajibu wao kama ipasavyo.

- Kama kiongozi hakutimiza wajibu wake, ni jukumu la wananchi kumwondoa madarakani kwa kufuata Sheria kama vile kumpigia kura ya hapana. Kifungu cha 14 (4) cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji) Na. 8 ya mwaka 1982 kinaweza kutumika.

## Majukumu ya Mkutano Mkuu wa Kitongoji

Kisheria majukumu ya Mkutano Mkuu wa Kitongoji ni kama ifuatavyo:

- Kupokea na kujadili taarifa za utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Kitongoji zitakazowasilishwa na Mwenyekiti wa Kitongoji;
- Kujadili taarifa ya utekelezaji wa mikakati ya kupambana na umaskini;
- Kujadili hali ya ulinzi na usalama na maendeleo katika eneo la Kitongoji;
- Kuweka mikakati ya kupambana na ugonjwa wa UKIMWI;
- Kupokea maelekezo kutoka kwa Halmashauri ya Kijiji na kuweka mikakati ya utekelezaji wake katika Kitongoji.

Ifahamike kuwa pamoja na kushughulika masuala yanayohusu Kitongoji, Mkutano Mkuu unapaswa pia kutekeleza maamuzi yanayotokana na Halmashauri ya Kijiji. Kwa maana hiyo basi, Mkutano Mkuu wa Kitongoji ni muhimu sana katika utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya Kijiji. Pale ambapo mikutano hiyo inafanyika kuna mafanikio makubwa ya maendeleo.

## Wajibu na Majukumu ya Mkutano Mkuu wa Mtaa

Wajibu wa Mkutano Mkuu wa Mtaa ni kupokea na kujadili taarifa kuhusu:

- Miradi inayoendeshwa katika eneo la Mtaa na maendeleo yake;
- Hali ya usalama na ulinzi katika eneo la Mtaa;
- Matatizo ya huduma za jamii na hatua zilizochukuliwa;
- Maamuzi ya Kamati ya Maendeleo ya Kata au ya Halmashauri ya Mji, Manispaa au Jiji kupitia Kamati ya Maendeleo ya Kata yanayohusu Mtaa;
- Maamuzi ya Kamati ya Mtaa na utekelezaji wake;

- Suala lingine lolote linalohusu utoaji wa huduma na maendeleo ya kijamii na kiuchumi;
- Kumwondoa madarakani Mwenyekiti wa Mtaa inapodhihirika kwamba ameshindwa kumudu madaraka yake kwa kuzingatia sheria.

## Wajibu na Majukumu ya Mkutano Mkuu wa Kijiji

Wajibu na majukumu ya Mkutano Mkuu wa Kijiji ni pamoja na:

- Kupokea na kujadili taarifa za utekelezaji wa shughuli mbalimbali;
- Kupokea na kujadili mapato na matumizi ya fedha;
- Kupokea na kujadili taarifa za makusanyo ya fedha yakiwamo ya ushuru, ada na mapato mengine yanayopaswa kukusanywa ndani ya kijiji kwa mujibu wa sheria;
- Kupokea na kujadili taarifa za watu walioomba kupewa ardhi;
- Kupokea na kujadili mapendekezo yatakayotolewa na Halmashauri ya Kijiji au Kitongoji;
- Kupokea maagizo (kama yapo) kutoka ngazi za juu za Serikali na kuweka mkakati wa utekelezaji;
- Kufanya maamuzi yanayozingatia demokrasia;
- Kuchagua Mwenyekiti na Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji;
- Kujadili na kupitisha bajeti na mipango ya maendeleo ya Kijiji.

## Majukumu ya Kamati ya Maendeleo ya Kata

Kwa mujibu wa Kifungu cha 32 (1) cha Sheria za Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Na. 7 ya mwaka 1982 na Kifungu 16(1) cha Sheria za Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji) Na.8 ya mwaka 1982, majukumu ya Kamati za Maendeleo za Kata ni kama ifuatavyo:

- Kukuza uanzishaji na uendelezaji wa biashara na shughuli za ushirika katika Kata;
- Uanzishaji wa kazi au shughuli yenye lengo la kuleta ustawi wa jamii wa wakazi katika Kata;
- Kusimamia na kuratibu utekelezaji wa miradi na programu za Halmashauri ya Wilaya katika Kata;
- Kupanga na kuratibu shughuli na kutoa msaada na ushauri kwa

wakazi walio katika Kata ambao wanajihusisha na shughuli yoyote au biashara (halali ya aina yoyote);

- Kupendekeza kwa Halmashauri ya Kijiji au Wilaya utungaji wa sheria ndogo;
- Kufuatilia ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri;
- Kuanzisha na kuendeleza ushirikishwaji wa wananchi katika Maendeleo ya Kata;
- Kusimamia mifuko yote ya fedha iliyoanzishwa na kukabidhiwa kwa Kata;
- Kusimamia maafa na shughuli zinazohusu mazingira; na
- Kuendeleza masuala ya jinsia.

## Majukumu ya Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Jiji

- Kuandaa, kuratibu na kusimamia utekelezaji wa mipango ya maendeleo katika eneo la Halmashauri hiyo.
- Kusimamia na kuhakikisha kuwa watendaji wanatimiza wajibu wao. Ni jukumu la Halmashauri kufuatilia utendaji kazi wa watumishi wake hasa waliopo katika Kata, Mtaa na Vijiji.
- Kutunga sheria ndogo zitakazotumika katika eneo la Halmashauri hiyo na kupitisha sheria ndogo zitakazotungwa na Vijiji vilivyoko ndani ya Halmashauri hiyo.

# Hitimisho

Masuala yaliyoainishwa katika kijitabu hiki yanaonesha jinsi mfumo wa Serikali za Mitaa wa Tanzania unavyotoa fursa kwa wananchi katika kukuza demokrasia na katika kuchangia maendeleo yao. Ki msingi ni kweli kuwa Serikali za Mitaa zinapeleka madaraka kwa wananchi. Kwa kutumia fursa hizo mwananchi anaweza kufaidika kama ifuatavyo:

- Kushiriki kwa njia ya moja kwa moja kwa kuhudhuria na kuchangia hoja katika mikutano mikuu ya kisheria katika ngazi ya Kitongoji, Kijiji na Mtaa.
- Kushiriki moja kwa moja kama mjumbe kwenye kamati mbali mbali katika ngazi ya Kitongoji, Kijiji na Mtaa. Vijiji vingi vimekwishaunda kamati, kwa mfano Kamati za Elimu, Kamati za Maji, Kamati za Mazingira, Kamati za Ardhi, na nyinginezo ambazo wananchi wanaweza kushiriki kutoa maamuzi na kuyatekeleza.
- Kushiriki kwa njia ya uwakilishi kupitia wajumbe wa kuchaguliwa kama vile Diwani, Mwenyekiti wa Kitongoji, Kijiji au Mtaa au wajumbe wa Halmashauri za Kijiji na kamati za Kitongoji au Mtaa.
- Kutoa maoni kwenye masanduku ya maoni yaliyoko kwenye ofisi za Serikali za Mitaa katika ngazi mbalimbali.
- Pia anaweza kusoma mihutasari ya vikao mbalimbali kama inayowekwa kwenye mbao za matangazo katika ngazi mbalimbali za Serikali za Mitaa.

Izingatiwe kwamba bila wananchi kutumia fursa hizi, sio rahisi kupata haki zao za kimsingi kama vile:

- Kuchagua na kuchaguliwa kwa mujibu wa sheria na taratibu za uchaguzi.
- Kushiriki katika shughuli zote za kisiasa na kimaendeleo katika Kitongoji, Mtaa na Kijiji.
- Kujua mapato na matumizi ya fedha na rasilimali nyingine katika Kitongoji, Mtaa au Kijiji chake.
- Kufahamu mipango yote ya maendeleo inayoendeshwa na Kitongoji, Kijiji na Mtaa.

Changamoto kubwa kwa maboresho ya Serikali za Mitaa yanayoendelea nchini ni kuwawezesha wananchi kutambua kuwa mfumo na muundo wa Serikali za Mitaa ni fursa kwao na waitumie kikamilifu. Kijitabu hiki ni mchango mdogo katika changamoto hiyo.

Kijitabu hiki kimeandaliwa kwa kuzingatia maelezo yaliyoko kwenye kitabu kifuatacho:

*Jamhuri ya Muungano wa Tanzania: Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa:* **Mafunzo ya Awali ya Maafisa Watendaji wa Vijiji na Mitaa Tanzania Bara** *cha Mwaka 2004 Dodoma*

**PO-RALG**
Mlezi House
P. O. Box 1923
Dodoma
Tanzania
www.poralg.go.tz